JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barua pepe: rbckinondoni@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAKUKURU Mkoa,
S.L.P 90397,
Kinondoni

## TAARIFA KWA UMMA

**Kinondoni,**
**Januari 22, 2026**

## TAKUKURU YAWATAFUTA ALEX MSAMA MWITA NA BENNY MWITA SAMMOH KUJIBU MASHTAKA DHIDI YA RUSHWA

**Ndugu Wanahabari,**

Taarifa ninayoiwasilisha kwenu leo, inahusu kuwatafuta Washtakiwa **Alex Msama Mwita** na **Benny Mwita Sammoh** wanaokabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi ikiwemo kuongoza genge la uhalifu, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu pamoja na utakatishaji fedha kupitia Shauri la Uhujumu Uchumi na. **1371/2026**.

Shauri hili lilifunguliwa tarehe 21 Januari 2026 katika **Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu** mbele ya **Hakimu Mkazi Mkuu Hassan Makube**. Shauri hili ni matokeo ya uchunguzi wa tuhuma kuhusiana na kiwanja namba **33** kilichopo eneo la Vijibweni, Kigamboni mkoani Dar es Salaam, lenye hati namba **129621** iliyotolewa kwa **Africa Energy Limited Mwaka 2013**.

Washtakiwa tajwa hapo juu wanadaiwa kughushi hati ya mauziano ya eneo tajwa na kuwasilisha kwenye Baraza la Ardhi Wilaya ya Temeke ikionesha kuwa **Benny Mwita Sammoh** amenunua kiwanja hicho kutoka kwa **Mwinyikombo Wahela** huku wakijua kuwa sio kweli.

Kufuatia wasilisho hilo katika Baraza la Ardhi Temeke, **Benny Mwita Sammoh** kwa kutumia jina lingine la **Ben Samson** alifanikiwa kuuza eneo hilo kwa kampuni ya **World Oil Tanzania Limited** na kujipatia jumla ya Tsh. **984,000,000/=** kati ya Tsh **1,700,000,000/=** zilizoainishwa kwenye mkataba wa mauzo. Ushahidi uliopatikana unaonesha kuwa **Benny Mwita Sammoh** alihamisha jumla ya Tsh. **370,000,000/=** kati ya **984,000,000/=** kwenda kwa **Alex Msama Mwita** ikiwa ni sehemu ya fedha zilizotokana na mauzo ya kiwanja tajwa.

**Ndugu Wanahabari,**
Uchunguzi huu umefanywa na timu ya wachunguzi kutoka Ofisi ya TAKUKURU Kinondoni na TAKUKURU Temeke. Baada ya kukamilika kwake, washtakiwa tajwa walitakiwa kuripoti Ofisi ya TAKUKURU Kinondoni mwezi Desemba 2025 ili wafikishwe mahakamani jambo ambalo hawakulitekeleza.

Jitihada mbalimbali za kuwataka kufika zimefanyika bila ya mafanikio, hivyo tunaomba mwananchi yeyote mwenye taarifa za upatikanaji wao kutoa taarifa kwenye Ofisi yoyote ya TAKUKURU au kupiga simu namba **0738 150236. Zawadi nono itatolewa kwa atakayefanikisha**. Hati za kuwakamata zimeshatolewa na Mahakama ya Kisutu **tarehe 21 Januari 2026** na Shauri hili litatajwa tena **tarehe 25 Februari 2026.**

**Ndugu Wanahabari,**
Sambamba na mashtaka hayo, **Alex Msama Mwita** anatafutwa pia na TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni kwa ajili ya kujibu tuhuma za kughushi na uvamizi wa eneo la kiwanja namba **234**, kilichopo Regent Estate Mikocheni, wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam.

**Ndugu Wanahabari,**
TAKUKURU inatoa tahadhari kwa watumishi wa umma kutoshiriki katika vitendo vya kufanikisha watu kujipatia umiliki wa viwanja kwa njia ya udanganyifu. Aidha, wananchi wanatahadharishwa kupata taarifa sahihi kabla ya kufanya ununuzi wa viwanja hususani viwanja vilivyopo katika maeneo ya kimkakati (*strategic areas*).

Tunatoa rai kwa wananchi wote kuendelea kujiepusha na vitendo vya rushwa na kushiriki kikamilifu katika kuzuia vitendo hivyo katika maeneo yao. Vilevile, tunawasihi kuendelea kutoa ushirikiano kwenye uchunguzi na kushiriki kutoa ushahidi mahakamani pale inapohitajika kwani **Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu; Tutimize Wajibu Wetu!**

Imetolewa na:


ELIZABETH MOKIWA

**NAIBU MKUU WA TAKUKURU**
**(M) KINONDONI**

**SIMU: 0738 150 237**